

Maswali

1. Hadithi hii ilitokea wapi?
2. Zakayo alifanya kazi gani?
3. Mbona watu walimchukia?
4. Mbona Zakayo alipanda juu ya mti?
5. Yesu aliambia Zakayo nini?
6. Mbona watu walilalamika?
7. Zakayo aliambia watu nini walipokuwa kwa nyumba yake?
8. Yesu aliambia watu kwamba nini ilkuwa imekuja kwa nyumba ya Zakayo?
9. Tunajifunza nini kwa mfano wa hili somo la Zakayo?

Majibu

1. Hadithi hii ilikuwa Yeriko.
2. Alikuwa mtosha ushuru.
3. Alichukuwa pesa nyingi za ushuru na aliweka zingine.
4. Alikuwa mfupi sana hangeweza kuonea juu ya umati.
5. Kwamba ataenda kwa nyumba yake.
6. Hawakutaka Yesu akae na mwenye dhambi.
7. Alisema atapea maskini nusu ya mali yake na atarudisha yote aliyochukuwa kwa wizi.
8. Alisema wokovu ulikuwa umekuwa kwa nyumba ya Zakayo.
9. Tutafute Yesu hata tuwe na ugumu wa namna gani, tuwe tayari kuungama makosa yetu na tujirekebishe.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



35 Zakayo

Marejeo

Luka 19:1-10

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba ni lazima tumuheshimu Yesu kila siku.

Maneno maalum

1. Safari ya mwisho + Yeriko + umati
2. Mtu mfupi + ushuru wa Warumi + tajiri
3. Hakuna rafiki + hakupendwa
4. Umati njiani + Yesu anakuja
5. Mkuyu + panda + ona Yesu
6. Yesu alisimama + tengeneza + chakula + umati haukufurahia
7. Lipa tena + wokovu + okoa waliopotea
8. Tafuta Yesu kwanza + shinda majaribu

35.1 Yesu aliaenda Yerusalemu kwa safari yake ya mwisho akipitia njia ya Yeriko. Mji wa Yeriko ulikuwa kando ya bahari ya chumvi, na ulikuwa na shuguli nyingi. Yesu na wanafunzi wake walikwea huko kupitia njia ya mwamba. Walipokuwa wakipitia huko Yeriko, umati kubwa wa watu ulimzunguka Yesu ili wasikilize mafundisho yake.

35.2 Zakayo alikuwa mfupi wa kimo, tena watu walimdharau kwa sababu nyingine. Alikuwa amejiunga na jeshi la Warumi lililochukiwa na watu kwa kukusanya ushuru kutoka kwao. Hata si kwa kuchukua tu, lakini alichukua zaidi ili ajiwekee zingine. Hii ilimletea utajiri mwingi kwa sababu alifanya hivyo kwa mda mrefu. Aliishi maisha mazuri. Alikuwa na wafanyi kazi wengi. Alikula na kunywa vizuri hata na kuvaa nguo za hali ya juu.

35.3 Zakayo hakukuwa na marafiki wa kweli. Watu wataifa lake walimchukia na Warumi walitaka tu kumtumia. Utajiri wake ulifanya watu wasikuwe wazuri kwake. Alipokuwa akitembea njiani, watu hawangeenda upande wake badala yake walieende upande mwingine, hawakutaka wazungumze naye. Wangemuonyesha vidole na kumsengenya nyuma yake.

35.4 Zakayo alijikuta ako kando ya njia ya umati uliokuwa ukija. La ajabu kwa mara ya kwanza watu hawakutabua uwepo wake. Walikuwa wakizungumzia juu ya Yesu aliyekuwa akija. Zakayo alitaka sana kumuona Yesu lakini kwa sababu ya ufupi wake hangeweza, hata alisukumwa kwa chuki. Alijaribu tena lakini hakuna aliyetaka apite.



35.5 Ghafula akawa na shauri la kufanya. Mbele yake kulikuwa mkuyu uliokuwa umetokezea juu njiani. Alikimpia na kupanda juu kwa tawi moja. Kufikia hapa, nguo zake za kifahari zilikuwa zimechafuka lakini kutoka kwa alikokuwa, aliweza kumuona Yesu katikati ya umati mkuu akija.

35.6 Yesu alisimama chini ya mti na kuangalia juu alikokuwa Zakayo. Alimwambia ashuke chini na aende nyumbani kwake amtengenezee yeye na wanafunzi wake chakula wale kwa hiyo siku. Zakayo alitambaa chini kwa haraka akiwa na furaha na akakimbia nyumbani. Wafanyikazi walichukuwa mda mfupi kutengenezea Yesu na marafiki wake karamu kubwa na kuwakaribisha nyumbani kwake. Watu wengine walilalamika mbona Yesu anayetakiwa aelewe saidi alikula na wenye dhambi kama Zakayo. Walifikiri kwamba ikiwa Yesu anajua angekuwa mtu wa kwanza kumshutumu.

35.7 Karamu ilipokuwa ikiendelea, Zakayo alisimama na kuwanyamazisha watu wote. Aliangalia Yesu na akamwambia kwamba kutokea siku hiyo angechukuwa nusu ya mali yake na agawe masikini, na kwa yeyote aliyekuwa amemnyang'anya mali yake, angemlipa mara nne. Yesu alifurahi na kusema kwa sauti ili kila mtu asikie kwamba wokovu ulikuwa umekuja kwa Zakayo na kwa watu wote wa nyumba yake kwa sababu ametubu dhambi zake na amekubali kujirekebisha. Yesu alikuja kutafuta na kuokoa watu kama Zakayo waliokuwa wamepotea.

35.8 Ingewezekana Zakayo asizumbukane kutafuta Yesu. Badala yake aliharibu nguo zake akipanda juu ya mti. Angekataa Yesu asiende kwa nyumba yake. Badala yake alitumia pesa nyingi kwa Yesu na wanafunzi wake alipowakaribisha nyumbani kwake. Tena baada ya hayo hangefanya lingine lolote badala yake, alijua ako na makosa upande wa pesa. Aliamua kuzirudisha zote. Tukimtafuta Yesu, tusikubali jambo lolote lituzuie kama vile Zakayo hakukubali ufupi wake umzuie kuona Yesu. Yesu atatutafuta tukitaka atupate. Yesu akitaka tumhutumie tutajua udhaifu wetu na lazima tuwe tayari kujitolea kwa hali zote ili tupate wokovu.